JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO

# TANGAZO

**29.07.2025**

## MWALIKO WA MAFUNDI UJENZI KWENYE KIKAO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA CHAMWINO ANAPENDA KUWAALIKA MAFUNDI WOTE WENYE UJUZI WA KUJENGA MAJENGO MBALIMBALI YA SERIKALI KATIKA KIKAO KITAKACHOFANYIKA SIKU YA JUMANNE TAREHE **05.08.2025 SAA NNE ASUBUHI**, KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA CHAMWINO.

**DHUMUNI LA KIKAO HICHO NI PAMOJA** NA KUTAMBULISHA MIRADI MBALIMBALI ILIYOPOKELEWA KATIKA HALMASHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026, MIKAKATI MBALIMBALI INAYOHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA SERIKALI IKIWEMO USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA MIKATABA YA UJENZI.

AIDHA, KUTAKUWA NA USAJILI WA MAFUNDI KWENYE MFUMO WA UNUNUZI SERIKALINI (NEST) KWA MAFUNDI WASIOSAJILIWA, KUELEKEZWA NAMNA YA UJAZAJI WA ZABUNI ZA UFUNDI KWENYE MFUMO, VIGEZO NA MASHARTI KATIKA MIKATABA YA MAFUNDI, PAMOJA NA MASUALA MBALIMBALI YANAYOHUSIANA NA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA SERIKALI.

**MAHITAJI MUHIMU YA USAJILI KATIKA MFUMO NI PAMOJA NA BARUA YA UTAMBULISHO KUTOKA OFISI YA SERIKALI YA KIJIJI/MTAA AU VYETI VYA UFUNDI KUTOKA KATIKA VYUO VINAVYO TAMBULIKA NA SERIKALI , ANUANI YA BARUA PEPE (Email address), PAMOJA NA NAMBARI YA TIN. KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBARI YA SIMU NA. 0713564311.**

**NYOTE MNAKARIBISHWA.**

**LIMETOLEWA NA,**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W) CHAMWINO**